



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA BAGAMOYO



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb Na: BAG/LD/12534/13

Tarehe: 13 Februari, 2025


Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
S.L.P 938,
DAR ES SALAAM.

Yah: **OMBI LA MAREKEBISHO YA NAMBA YA KIWANJA KATIKA CHETI CHA UWEKEZAJI WA KIWANJA NA. 272 KEREGE KUWA KIWANJA NAMBA 332 KITALU A KEREGE, WILAYA YA BAGAMOYO.**

Husika na somo hilo hapo juu.

2. Rejea barua yenye Kumb.Na. LD/313175/30 ya tarehe 21 Novemba, 2024 kutoka kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Pwani na Ofisi yenu kupewa nakala. Barua hiyo inahusiana na kurejesha miliki ya kiwanja Na.272 Kerege na kutangaza kiwanja hicho kwa ajili ya uwekezaji.
3. Aidha, maudhui ya barua hiyo, yalikuwa yanahusiana na ombi lililowasilishwa na Kampuni ya **Rostar Vehicle Equipment Limited** la kuomba eneo walilolinunua linalopakana na kiwanja Na.272 kuunganishwa katika upimaji mmoja.
4. Baada ya marekebisho ya mchoro wa mipangomiji kufanyika, upimaji wa kiwanja Na.272 Kerege ulifutwa na eneo hilo lilipimwa upya kwa kujumuisha eneo lote na kuwa kiwanja Na.332 Kitalu A Kerege.
5. Kampuni hiyo imewasilisha ombi la kumilikishwa kiwanja kwa njia ya uwekezaji kupata haki isiyo ya asili lakini Ofisi imeshindwa kufanyia kazi ombi hilo kutokana na kukosekana kwa Cheti cha Uwekezaji chenye namba ya kiwanja Na.332 Kitalu A Kerege kutoka Ofisi yenu.
6. Kwa barua hii, tunawasilisha ombi hilo katika Ofisi yenu kwa hatua zaidi.




 Shauri Selenga
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
BAGAMOYO

Nakala: Kamishna wa Ardhi,
 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,
 Mji wa Serikali Mtumba,
 S.L.P 2908,
40477 DODOMA.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Pwani,
 S.L.P 9230,
DAR ES SALAAM.

Mkurugenzi Mtendaji,
 Roster Vehicle Equipment Limited,
 S.L.P 13989,
DAR ES SALAAM.

MKURUGENZI MTENDAJI
ROSTER VEHICLE EQUIPMENT LIMITED
S-L-P 13989
DAR-ES-SALAAM

